IDYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

MICRO CREDIT SACCOS LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

MCHAKATO WA MIKOPO

Mwombaji kufika ofisini au kwa Kiongozi wa kikundi/Kanda ili kupata maelekezo juu ya Mikopo ya IDYDC na nini anatakiwa kufanya ili kupata Mkopo ikiwa atakuwa na sifa ya kukopeshwa.

1. Mwombaji akiona ana sifa atanunua fomu ya maombi ya Mkopo toka ofisini au kwa Kiongozi wa kikundi na kupata maelekezo ya jinsi ya kuijaza pamoja na viamabatanishi vinvyotakiwa.
2. Mwombaji ataenda kuijaza fomu ya maombi kwa kushirikiana na wanafamilia/mwenza wake (Mme & Mke) na wadhamini wake.
3. Mwombaji ataipeleka fomu ya maombi na viambatanishi vyote kwa Mwenyekiti wa Mtaa au Kijiji wa sehemu anayoishi Mwombaji kwa ajili ya utambuzi na kupitishwa.
4. Mwombaji atairudisha fomu ofisini au kwa Kiongozi wa kikundi pamoja na viambatanisho vyote vinavyotakiwa.

[DYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

MICRO CREDIT SACCOS LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

MCHAKATO BAADA YA KUIPOKEA FOMU OFISINI

1. Afisa Mikopo / Meneja ataipitia fomu ya maombi na akiona imekamilika atapanga ratiba ya kumfikia mwombaji.
2. Afisa Mikopo/Meneja atamtembelea mwombaji ili kupata uhakika wa taarifa za mwombaji na ukaguzi wa Makazi yake na dhamana za Mkopo pia atakagua biashara/mradi anao ombea mkopo. (Au Viongozi wa kikundi kwa maelekezo ya Meneja)
3. Afisa Mikopo/Meneja atatoa maoni kwenye fomu ya mwombaji na kuipeleka kwenye Kamati ya Mikopo au Bodi ya Wakurugenzi kwa hatua inayofuata.
4. Kamati ya Mikopo au Bodi ya wakurugenzi itapitia taarifa za mwombaji pamoja na maoni ya Afisa Mikopo/Meneja na Mwenyekiti wa Kijiji au Mtaa / pia maoni ya viongozi wa kikundi kama anatoka kwenye kikundi.
5. Kamati ya Mikopo/Bodi ya Wakurugenzi itatoa majibu ya maombi ya kukubaliwa au kukataliwa na hata kutakiwa kufanya marekebisho ya maombi yake kabla ya Mkopo.
6. Afisa Mikopo/Meneja atamjulisha mwombaji kwa maandishi au kwa njia ya simu majibu toka Kamati ya mikopo/ Bodi ya Wakurugenzi.
7. Aliyefanikiwa kupata Mkopo ataitwa ofisini pamoja na wadhamini kwa ajili ya kupata mafunzo mafupi ya ujasiriamali na mikopo na baada ya mafunzo watasaini Mkataba wa mkopo.
8. Walio saini Mikataba wa Mikopo watapewa Mikopo na maelekezo mafupi juu ya taratibu za ulipaji wa Mkopo

IDYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

MICRO CREDIT SACCOS LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

MUDA WA MCHAKATO TOKA KUPOKELEWA FOMU YA MAOMBI YA MKOPO OFISINI HADI KUPATA MKOPO AU MUDA WA KUPATA MAJIBU YA KUKATALIWA NA AU KUTAKIWA KUFANYA MAREKEBISHO

1. Aliyetizimiza vigezo vyote vya kupata Mkopo atapata Mkopo wake ndani ya siku saba za kazi na haitazidi siku kumi nanne ikiwa itakuwa amekamilisha taratibu zote za mafunzo na kusaini Mkataba kwa kuzingatia vigezo na masharti kwa huduma ya ndogo ya fedha.
2. Mwomnbaji aliye kataliwa atapewa majibu yake ndani ya siku saba za kazi kuwa ombi lake limekataliwa na ataambiwa sababu za kukataliwa.
3. Mwombaji mwenye mapungufu naye atapata majibu ndani ya siku saba ili aweze kufanyia kazi mapungufu yake ikiwa ataweza kufanyia marekebisho na ataleta marekebisho yake ofisini na siku ya kuleta marekebisho ndio siku itakayo hesabika kupokelewa fomu ofisini.
4. Mwombaji ambaye hataridhika na majibu yake ya maombi ataruhusiwa kukata rufaa kwa maandishi kwenda kwa Mwenyekiti wa Bodi ya IDYDC Microcredit ndani ya siku saba za kazi baada ya kupata majibu yake.

IDYDC MICRO CREDIT

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

BAADHI YA MIRADI AU BIASHARA ZINAZOWEZA KUPATA MIKOPO

1. Ushonaji kama vile nguo, viatu na ufumaji.
2. Usindikaji wa Mbogamboga, Matunda, Nyama. Maziwa na Nafaka.
3. Useremala, Uchongaji, Uchomeleaji (Welding).
4. Ufugaji kama vile:- Kuku, Nguruwe, Ng'ombe, Mbuzi, Sungura na Nyuki.
5. Uhunzi, Ufinyanzi na Ususi.
6. Utengenezaji wa Matofali na Mapambo (Vigae).
7. Kilimo cha muda mfupi na kidogo kidogo (wakulima wadogo wadogo) kama vile: Nyanya, Viazi, mbogamboga, vitunguu n.k. Kilimo cha bustani/Umwagiliaji.
8. Ufundi Simu, Redio, Pikipiki, Magari, Bajaji, Baiskeli, Umeme, Computer nk.
9. Ufundi Ujenzi, Upauaji,Uchoraji,Rangi nk.
10. Huduma ya mafunzo ya Elimu mbalimbali kama vile Computer, Simu, Ushonaji, Useremala, Umeme, Uaishi, Uungaji vyuma(Welding), Ufumaji, Uhunzi na Ususi.

11. Huduma za Fedha mitandao kama (Mpesa, Tigo pesa, Aitel maoney, Haltel money).
12. Mama lishe na Baba lishe
13. Migahawa, Cafe, Nyama choma, Chips nk
14. Viosk, vigenge, grocery.
15. Uuzaji nguo za Mitumba, nguo Mpya nk
16. Uuzaji nafaka, matunda, mbogamboga, Samaki, nyama nk.
17. Maduka madogomadogo ya vitu mbalimbali.
18. Usafirisha wa Bodaboda, Bajaji, Tax nk.
19. Miradi ya Vikundi vya Usafi, Mapishi, Mapambo, Michezo nk.
20. Maduka ua madawa ya binadamu na Mifugo.
21. Maduka ya Vyakula vya Mifugo.
22. Maduka ya vifaa vya Shule na Ofisi.
23. Saluni za Kike na Kiume.
24. Uchimbaji na uuzaji wa madini, Mchanga, Kokoto.
25. Uuzaji wa Mbao, Milunda, Kuni, Mkaa, Mabanzi nk.
26. Utengenezaji wa Sabuni, Keki, Vitafunwa.
27. Utengenezaji wa viatu na ung’alishaji Viatu, uuzaji wa viatu, Mabegi nk.

IDYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

MICRO CREDIT SACCOS LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

ACTIVITIES FINANCED AS CATEGORIZED BY IDYDC MICROCREDIT

1. **Agro-processing:**
   Fruits or vegetable processing, Meat canning, Milk processing, Oil extraction/processing etc.
2. **Manufacturing:**
   Carpentry, Blacksmith, Goldsmith, Cloth making, Handcraft, Brick making etc.
3. **Training/Retail Loans:**
   Vending, Food, Water, Cloth shop, Kiosk, Fruits.
4. **Service loan:**
   Saloon, Barbershop, Drugs store, Transport, Housing etc.
5. **Livestock/Crops:**
   Crops production Farming in small scale) Animal production (Livestock keeping) etc.
6. **Fishing Industry:**
   Fishing equipments and other related accessories.
7. **Mining/Quarrying:**
   Quarrying production and Mining extraction etc.

IDYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

VIAMBATANISHI KWENYE FOMU YA MAOMBI YA MKOPO

1. Picha mbili passport size za mwombaji.
2. Picha mbili kubwa za mwombaji na wadhamini wake. Picha moja wasimame kwenye mradi na nyingine kwenye dhamana za Mkopo.
3. Fomu ya kiapo cha dhamana ya Mkopo na ya kiapo cha mwenza (Mke/Mme ikiwa hayumo kwenye fomu ya maombi ya Mkopo (kiapo kiwe na picha passport size ya Mwenza anaye apa.)
4. Uthibitisho wa umiliki wa dhamana zinazo dhamini Mkopo. (Kama vile Kadi, Hati, Mkataba, Risti nk). Uthibitisho uwe halisi (Orignal).

NB: i. Fomu zote na picha zitapitishwa kwa Mwenyekiti wa Kijiji au Mtaa na zigongwe mhuri na saini ya mpitishaji.

ii. Wakati wa kusaini Mkataba Mwombaji na Wadhamini watatakiwa kufika na vitambulisho vyao vya NIDA, Uchaguzi (NEC), lessen ya dereva, Pass port (Hati ya kusafiria).

IDYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 **www.idydc.or.tz** Email: idydc.42@hotmail.com

HATUA ZA MIKOPO IDYDC MICRO CREDIT& SACCOS LTD.

HATUA	KIWANGO CHA MKOPO KINACHOWEZA KUOMBWA
1	50,000.00 – 300,000.00
2	300,000.00 – 600,000.00
3	600,000.00 – 1,000,000.00
4	1,000,000.00 – 1,500,000.00
5	1,500,000.00 – 2,000,000.00
6	2,000,000.00 – 3,000,000.00
7	3,000,000.00 – 4,000,000.00
8	4,000,000.00 – 5,000,000.00
9	5,000,000.00 – 7,000,000.00
10	7,000,000.00 – 9,000,000.00

11	**9,000,000.00 – 10,000,000.00**
12	**10,000,000.00 – 12,000,000.00**
13	**12,000,000.00 – 14,000,000.00**
14	**14,000,000.00 – 15,000,000.00**

IDYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

UTOAJI WA MIKOPO NA TAARIFA YA KUKATALIWA KUPEWA MKOPO

Utoaji wa Mikopo kwa walengwa.

IDYDC Microcredit itatoa Mikopo kwa wote wenye sifa ya kupata Mikopo kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukopesha na kwa kuzingatia sera ya mikopo bila kuathiri sheria ya Huduma ndogo za fedha na Kanuni za huduma ndogo za fedha zinazosimamia Taasisi ndogo za fedha za mwaka 2019.

VIGEZO VYA KUPATA MKOPO IDYDC MICRO CREDIT & SACCOS LTD (SIFA)

Ili kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha Mikopo inatole wa, baadhi ya mambo yafuatayo yatazingatiwa kabla ya Mkopo kutolewa kwa Mwombaji, na ni lazima Mwombaji huyo awe na vigezo (sifa) zifuatazo;

a. Awe na mradi, biashara au huduma anayotaka kukopea inayo kubalika kwa mjibu wa sheria za Nchi yetu.
b. Awe na vibali vyote vinavyotakiwa katika kufanya biashara/huduma hiyo (Awe tayari kuonyesha ushahidi unaothibitisha kuwa biashara/mradi anao ombea ni wake.)
c. Awe na umri wa miaka 18 hadi 70 na mwenye akili timamu na mwenye uwezo wa kufanya kazi.
b. Biashara/huduma inayo ombea Mkopo iwe kwenye eneo linalofikiwa na mradi wa Mikopo ya IDYDC.

c. Awe anafahamika na kutambuliwa na Serikali ya Kitongoji, Kijiji au mtaa kwa makazi yake na kazi zake za kiuchumi anazozifanya.
d. Asiwe na Mkopo alio shindwa kulipa wakati wa kuomba Mkopo mwingine.
e. Asiwe na Mkopo alioshindwa kulipa kutoka taasisi nyingin e.
f. Awe na historia nzuri katika urejeshaji wa Mikopo yake ID YDC na Taasisi nyingine.
g. Awe tayari kushiriki vizuri mafunzo ya Ujasiriamali na Mikopo ya takayotolewa na IDYDC kabla ya Mkopo.
h. Awe na mradi, biashara au huduma inayo tengeneza au inayotegemea kutengeneza faida.
i. Awe na dhamana toshelevu mara 2 ya Mkopo anao omba kwa ajili ya kudhamini Mkopo
j. Awe na wadhamini wasio pungua 2 wenye mali za kutosha kumdhamini Mkopajii.
j. Awe anatii na kufuata taratibu na sheria zote zilizo wekwa na Serikali katika uendeshaji mradi, biashara au huduma.
k. Awe ana heshimu na kuzingatia haki za binadamu na hasa watoto na mwenye historia nzuri ya kutunza watoto kwa kuwapa mahitaji ya Msingi. (Elimu, Afya, Chakula, Malazi, Mavazi)
l. Awe tayari kumshirikisha mwenza wake (Mke & Mme) kwenye fomu yake ya maombi ikiwa anaye.

IDYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

MICRO CREDIT SACCOS LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

GHARAMA ZA MIKOPO

1. Fomu ya maombi sh. 5,000/= Ofisini na sh 10,000 kwa kiongozi wa kikundi ambayo hairudishwi baada ya fomu kununuliwa.
2. Ada ya Mkopo ni 2% ya Mkopo.
3. Kinga ya Majanga ni 0.5% ya Mkopo.
4. Riba ya Mkopo 15%(Reducing balance.)
5. Faini ya kuto rejesha ni 50% ya rejesho lililocheleweshwa kwa Wiki/Mwezi
6. Kupigiwa simu ya kudai marejesho yaliyo cheleweshwa faini yake sh. 3,000/= kwa simu.

IDYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

MICRO CREDIT SACCOS LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 **L. NO: MSP2-0125** P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

KINGA DHIDI YA MAJANGA YA MIKOPO INALIPIA MAMBO MAKUU MATATU TU.

1. Ikiwa Mkopaji amefariki akiwa hajamaliza Mkopo na IDYDC imethibitisha kuwa kwa namna yeyote ile Mkopo ulio achwa hauwezi kulipwa tena na yeyote au wadhamini wake.
2. Ikiwa Mkopaji amepata ulemavu na imepelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kumwingizia kipato na hatimaye kushindwa kulipa Mkopo anaodaiwa kwa namna yeyote ile yeye au wadhamini wake.
3. Ikiwa Mkopaji amerukwa na akili na hawezi kutoa ushirikiano katika kufanya marejesho kwa mujibu wa Mkataba wake na daktari wa Serikali amethibitisha kuwa Mkopaji mhusika ana ugongwa wa afya ya akili na hali wadhamini wake hawana uwezo wa kulipa.

DHAMANA ZA MIKOPO ZINAZOKUBALIKA.

Kiasi cha Mkopo	Tarabu za kuomba	Dhamana zinzokubalika
50,000.00 – 3,000,000.00=	Fomu ya maombi ya Mkopo na viambatanisho vinavyotakiwa kama vile Picha, Hati ya Kiapo, Nyaraka za kumiliki Dhamana na ushahidi wa Dhamana na Biashara/Mradi kama wako.	Dhamana ziwe mara mbili ya Mkopo unaoombwa. Kama vile, **sofa, friji, Kabati, TV, Redio, Subwoofer,** **Cherehani, kiwanja, shamba, nyumba na vingine kwa makubaliano na ofisi.**
3,050,000.00 – 15,000,000.00	Fomu ya maombi ya Mkopo iambatane na Andiko dogo (fupi) la Mradi/Biashara viambatanishi vya ushahidi wa Mradi/Biashara/Nyaraka za Dhamana za Mikopo.	Dhamana ya mali isiyo hamishika iwe mara mbili ya Mkopo unaoombwa inaweza kuwa **Nyumba, Kiwanja, Shamba nyingine kwa makubaliano ya Ofisi (Mkopeshaji).**

IDYDC- MICRO CREDIT & SACCOC LTD

TEL: + 255 – 0755 – 626266 Reg. No: IR -633 P.O. BOX 795 IRINGA
FAX: + 255 – 026 – 2703112 www.idydc.or.tz Email: idydc.42@hotmail.com

SIFA ZA KUJIUNGA NA IDYDC SACCOS LTD

- Fungamano la pamoja katika chama ni kuwa mwanachama wa IDYDC na wanufaika wake.

SIFA ZA KUJIUNGA

1. Kuwa na umri wa miaka isiyopungua 18.
2. Uwe Mtanzania.
3. Uwe na tabia nzuri na mwaminifu.
4. Uwe na akili timamu.
5. Uwe umelipa kiingilio, umenunua Hisa na kuweka Akiba.
6. Uwe tayari kushiriki shughuli za chama.
7. Uwe tayari kuelewa na kutekeleza madhumuni ya chama.
8. Uwe tayari kufuata mashrti ya chama, kanuni na sheria za vyama vya ushirika.
9. Usiwe na shughuli inayofanana ya kuweka na kukopesha wanachama ili kuondoa mgongano wa masilahi.

UTARATIBU WA KUJIUNGA

1. Mwenye sifa sharti No 10 ataomba kwa kujaza fomu ya maombi ya kujiunga na chama.
2. Maombi ya tajadiliwa na Bodi ya chama. (kukubali au kukataliwa).
3. Bodi itapeleka pendekezo Mkutano mkuu kwa wale waliokubaliwa (uamuzi wa Mkutano mkuu utakuwa wa mwisho).
4. Ikiwa atakubaliwa atatakiwa kulipa Kiingilio, kununua Hisa, kununua Masharti.

WALIO KATALIWA

1. Bodi itawaandikia barua ya kuwajulisha na kueleza sababu.
2. Mwombaji anaweza kukata rufaa kwa maandishi kwa Mkutano mkuu.

KIINGILIO, HISA NA AKIBA

1. Kiingilio cha uanachama hadi sasa ni sh. 20,000/=
2. Hisa moja ni sh 10,000/= mwanachama anatakiwa kuwa na Hisa 20 yenye thamani ya sh 200,000/= mwaka wa kwanza Hisa 10 na wa pili Hisa 10, lakini unaweza kununua zote mwaka wa kwanza kama unaweza. Pia unaweza kununua zaidi ya 20

lakini hauruhusiwi kumiliki hiza moja ya tatu ya Hisa zote za wanachama.

3. Kuweka akiba za sh 10,000/= kila mwezi kwa ajili ya maendeleo ya Chama, pia akiba zinaweza kutumika kama dhamana ya Mkopo.

KUKOMA UANACHAMA

a. Kujiuzulu baada ya kutoa taarifa ya maandishi kwa Bodi kwa muda wa siku 60.
b. Kufukuzwa uanachama na wanachama katika Mkutano mkuu.
c. Kutenda kosa ambalo limetajwa katika sheria ya vyama vya ushirika, kanuni na masharti ya chama.
d. Kuto miliki Hisa kwa mujibu wa masharti haya.
e. Kuto hudhuria Mikutano mikuu mitatu mfululizo bila taarifa ya maandishi.
f. Kutoa au kupokea Rushwa kwania ya kupata upendeleo.
g. Kupata na ugonjwa wa akili (kichaa) kilicho thibitishwa na Daktari wa Serikali.
h. Kukoma kuwa raia wa Tanzania.

KUFUKUZWA UANACHAMA

a. Kutotekeleza ahadi alizotoa katika chama.
b. Sababu zilizotajwa kanuni ya 39 (2) ya vyama vya Ushirika 2015.
c. Kutotekeleza maazimio yaliyotolewa na kukubaliwa katika Mkutano mkuu.
d. Kuto shiriki shughuli za chama kwa muda wa miezi 6 mfululizo.
e. Kushindwa kurejesha kwa muda uliopangwa bila sababu inayokubalika na Mkutano mkuu.
f. Kushindwa kuweka akiba kama ilivyo kwenye masharti ya chama sera ya Mikopo kama itakavyo elekezwa kwenye sheria ya vyama vya Ushirika.